



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUREJESHA RATIBA ZA MABASI 38 YA KAMPUNI YA NEW FORCE  
KUANZA SAFARI MUDA WA SAA 9.00 USIKU NA SAA 11 ALFAJIRI**

***Dar es Salaam,***

***Tarehe 08, Septemba, 2023.***

Mnamo tarehe 03 Julai, 2023 Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilisitisha ratiba za mabasi ya kampuni ya NEW FORCE kuanza safari muda wa saa tisa (9:00) usiku na saa kumi na moja (11:00) alfajiri kutokana na ukiukwaji wa masharti ya leseni za usafirishaji hasa kutoka kabla ya muda uliodhinishwa, mwendokasi, na matukio ya ajali za mfululizo. Mamlaka ilisitisha leseni za mabasi hayo na kutoa maelekezo yafuatayo:-

- i. Mabasi yote yaanza safari muda wa 12.00 asubuhi;
- ii. Kutafuta mshauri mwelekezi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa;
  - a) uongozi wa kampuni kuhusiana na masuala ya usalama, kuwa na mpango kazi wa matengenezo ya mabasi na usimamizi wa masharti ya leseni za usafirishaji wa abiria na;
  - b) Kutoa mafunzo kwa madereva wote wa kampuni juu ya kanuni za LATRA, Sheria za Usalama Barabarani na Udereva wa Kujihami and udhibiti wa uchovu (*Fatigue Management*).
- iii. Kuhakikisha kuwa madereva wote wanasajiliwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa magari (VTS), kuwa na i-button na kusajiliwa kwenye mfumo wa uthibitisho wa madereva.

**Baada ya kampuni hii kupewa adhabu hiyo**, Kampuni hii ilishirikisha Jeshi la Polisi, LATRA na mshauri mwelekezi katika kutekeleza maagizo ya Mamlaka, ambapo Jeshi la Polisi lilishiriki kutoa mafunzo ya Sheria ya Usalama Barabarani, LATRA ilihusika katika

kutoa elimu ya Masharti ya leseni za usafirishaji magari ya abiria na mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa magari na usajili wa madereva.

Kwa sababu hii Mamlaka imejiridhisha kampuni hii kutekeleza yafuatayo:-

1. Kupokea taarifa ya mafunzo yaliyotolewa kwa madera 50 wa kampuni hiyo kwa kuona vyeti vya kuhitimu mafunzo;
2. Tumepokea orodha ya wadhamini wa madereva hao kuwa wamesoma wameelewa na watazingatia Sheria zote za Usalama Barabarani katika kutoa huduma za usafirishaji abiria;
3. Tumefuatilia kwenye mfumo wa VTS mabasi yote ya kampuni hiyo kwa kipindi chote cha adhabu na kujiridhisha kuwa uvunjifu wa ratiba kwa kutoka kabla ya muda na mwendo kasi umedhibitiwa. Hii ni dalili njema kwa uongozi na madera wa kampuni hii kutii Sheria.

Kwa sababu hii, Mamlaka inaamua kurudisha ratiba na leseni kwa mabasi yote 38 kuanzia tarehe 11 Septemba, 2023 ya muda wa 9.00 usiku na saa 11.00 alfajiri.

Aidha, kutolewa kwa ruhusa hii iwe ni fundisho kwa kampuni hii na wasafirishaji wote wanaokiuka sheria na taratibu za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kwenda mwendo kasi, kuchezea vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi, kutoka kabla ya muda au kutoa huduma za usafirishaji abiria bila kufuata utaratibu na makosa mengine kwa makusudi au kwa uzembe. Mamlaka inaendelea kufuatilia kwa ukaribu utendaji wa kampuni hii pamoja na watoa huduma nyingine.

Iwapo Mamlaka itabaini uvunjifu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za utoaji huduma za usafiri wa abiria kwa mtoa huduma yeyote, haitasita kuchukua hatua stahiki.

**Imetolewa na;**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**